TANGAZO LA SERIKALI NA. 466 la tarehe 7/6/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

---

# SHERIA NDOGO

---

*(Imetengenewa chini ya kifungu cha 153(1))*

SHERIA NDOGO YA AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA UVINZA ZA MWAKA 2024.

Jina

1.Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Afya na Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza za Mwaka 2024.

Matumizi

2.Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa pale ambapo muktadha utaelekeza vinginevyo:

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chakula" maana yake ni kitu chochote kinacholiwa au kunywewa na binadamu isipokuwa madawa;

Sura ya 331

"chanzo cha maji" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"kitakasa mikono" maana yake ni sabuni au kemikali ambayo inatumika kuangamiza vidudu na virusi wa aina mbalimbali katika mikono.

"kizimba cha taka" maana yake ni kizimba cha taka au chombo maalum kilichowekwa na Halmashauri kwa ajili ya jamii kuhifadhia taka ngumu kabla ya kuzisafirishwa hadi kwenye jalala kuu lililoidhinishwa na Halmashauri;

Sura ya 191

"maji taka" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"mkazi" maana yake ni mtu yeyote ambaye kwa kawaida anaishi kwenye eneo lililoko ndani ya Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri;

"mtoa huduma" ni mfanyakazi kwenye sehemu za biashara zinazotoa huduma ya chakula, malazi au vinywaji mbalimbali;

Sura ya 287

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Serikali za Mita ana Mamlaka za Wilaya.

Sura ya 191

"taka" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura ya 191

"taka ngumu" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"Ushuru wa uzoaji taka" maana yake ni malipo yanayotozwa na Halmashauri kwa ajili ya huduma ya uzoaji taka;

"wakala "maana yake ni, kampuni, taasisi, kikundi au mtu binafsi aliyeteuliwa na halmashauri kwa ajili ya kutoa huduma ya kuzoa taka;

"Wanyama" maana yake ni ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe, punda, mbwa pamoja na wanyama wengine wafugwao.

Wajibu wa kufanya usafi wa Mazingira

4.Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi anayeishi, anayemiliki eneo la nyumba, kiwanja au biashara kuhakikisha kwamba-

(a) mazingira yanayozunguka eneo lake yanakuwa safi wakati wote;
(b) taka zote zinakusanywa na kuondolewa kwa njia itakayoelekezwa na Halmashauri;
(c) anachimba shimo la kutupia taka litakalokuwa na urefu usiopungua kimo cha futi tatu na upana usiopungua futi mbili;
(d) anajenga choo imara cha kudumu kwa matofali na kuezeka kwa bati, tembe, majani, vigae chenye mlango unaofunga na kufunguka na kuhakikisha kwamba choo kinatumika wakati wote na kuwe na chombo cha maji tiririka na sabuni ya kunawa mikono;
(e) eneo lake halina mazalia ya mbu, panya na wadudu wengine hatarishi;
(f) maji yote yanayotumika kwa kunywa ni safi na salama bila kujali yametoka kwenye chanzo gani cha maji;
(g) kuwa na chombo chenye maji tiririka pamoja na kitakasa mikono mbele ya sehemu ya biashara na kuhakikisha kuwa kila muhitaji huduma ananawa au kujitakasa mikono kabla ya kupata huduma.

Ilani ya kufunga au katazo au marekebisho

5.-(1) Halmashauri itatoa ilani kwa mwenye nyumba au mpangaji kumtaka arekebishe hali ya choo baada ya kugundulika kuwa nyumba yake au anayoishi haina choo au choo kilichopo kimejaa au hakifai kwa matumizi ya binadamu kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kufunga choo chochote ambacho kitaonekana kichafu au cha kuhatarisha maisha ya binadamu na hakitaruhusiwa kutumika mpaka Halmashauri itakaporidhika na matengenezo yaliyofanyika.

(3) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1)

Halmashauri inaweza kuamuru nyumba au jengo hilo lisitumike kwa shughuli za makazi au biashara au taasisi mpaka mmiliki wake atakapokuwa ametimiza maelekezo aliyopewa.

(4) Halmashauri itatoa ilani kwa mtu yeyote kama atagundua kuwa eneo alilokagua lina kero yoyote ili aondoe kero hiyo.

Uhifadhi wa maji taka

6. Kila mmiliki wa nyumba au kiwanda au eneo la biashara anatakiwa-

(a) kuhakikisha kuwa anakaro la kuhifadhia maji taka;

(b) kunyonya maji takakila wakati karo linapojaa;

(c) kutotiririsha au kutoelekeza maji kutoka vyooni, bafuni, karoni au viwandani kwenda barabarani, uchochoroni, mtoni, kwenye vyanzo vya maji, maeneo ya wazi, kwenye mfereji wa maji ya mvua au sehemu yoyote ambayo haijatengwa kwa ajili ya kuhifadhia maji taka; na

(d) kuhakikisha hasababishi harufu yenye madhara inayotokana na shughuli zinazofanyika katika eneo hilo.

Utengenezaji na uuzaji wa vyakula

7. Mtu yeyote anayetengeneza, kuchoma, kupika, kuchemsha au kuuza chakula cha aina yoyote katika eneo la Halmashauri atatakiwa-

(a) kutimiza masharti na kanuni za afya;

(b) kuwa na kibali kutoka kwa Afisa Afya wa Halmashauri;

(c) kuhifadhi vyakula katika chombo safi chenye mfuniko kinachozuia inzi, vumbi na wadudu waletao madhara kwa afya ya binadamu; na

(d) kuuza vyakula visivyopikwa vikiwa vimewekwa juu, ya meza au chombo

kisichoruhusu vyakula hivyo kuwa chini.

Ukaguzi na upimaji wa afya

8.-(1) Kila mfanyabiashara au mmiliki au mhudumu wa hoteli, migahawa, baa, nyumba za kulala wageni, bucha, waoka mikate, au watu wanaoshughulika na kuuza vyakula vilivyopikwa atahakikisha kwamba anapima afya kila baada ya miezi sita na kulipa ada ya upimaji kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(2) Halmashauri itahifadhi orodha ya majina ya watoa huduma wote ambao wamepimwa afya zao ili kurahisisha uhakiki wa afya za watumiaji hata kama mtoa huduma (mhudumu) au mfanyakazi amehama kwenda sehemu nyingine ndani ya Halmashauri aweze kutambulika kwa urahisi.

(3) Halmashauri itatoza ada ya ukaguzi wa afya ambayo italipwa kwa mwaka kabla ya mwombaji kupewa leseni ya biashara kama ilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

9.-(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kuingia katika eneo lolote ndani ya Halmashauri kuanzia saa moja na nusu asubuhi hadi saa tisa na nusu alasiri kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

(2) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kushauri au kuelekeza watu au mtu kutokuishi katika jengo ambalo linahatarisha afya au maisha ya watu na viumbe hai.

(3) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kuzuia shughuli mbalimbali wakati wa mlipuko wa magonjwa ikiwa pamoja na kukamata vyombo au vifaa vingine vinavyotumika na ambavyo vinaweza kuleta madhara kwa wakazi wa Halmashari.

(4) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kufunga au kuagiza kufungwa kwa biashara yoyote au jengo ambalo halijakaguliwa au lililokaguliwa na kukutwa limekiuka kanuni na masharti ya afya.

Ukaguzi wa jengo la biashara

10. Kila mfanyabiashara atakuwa na wajibu wa kuhakikisha jengo la biashara linakaguliwa na Afisa Mwidhiniwa kabla ya kuanzisha biashara.

Vifaa vya kuhifadhia taka ngumu

11.-(1) Kila mmliki wa jengo la makazi au mpangaji wa jengo la makazi au mtu yeyote anayefanyia biashara katika eneo lolote ndani ya Halmashauri atatakiwa kuwa na chombo cha kuhifadhia takataka chenye mfuniko na atawajibika kukusanya takataka hizo kwenye vizimba vya kuzolea takataka katika maeneo yaliyoainishwa.

(2) Kila mmiliki wa jengo au mpangaji wa nyumba iliyoko katika ukanda wa kijani, katika maeneo ambayo hayajapimwa atalazimika kuwa na shimo kubwa la kukusanyia taka ngumu katika eneo lake.

(3) Mtu yeyote anaemiliki au dereva wa chombo cha kusafirisha abiria atahakikisha kwamba anaweka chombo cha kuhifadhia taka zitakazozalishwa ndani ya chombo cha usafiri na kuzitupa katika sehemu maalum iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili hiyo.

Taratibu za kubomoa jengo

12.-(1) Mtu yeyote anaetaka kubomoa au kusababisha kubomoka jengo au sehemu ya jengo anatakiwa kuwa na kibali cha Halmashauri.

(2) Mtu yeyote atakayeomba na kupata kibali cha kubomoa jengo au sehemu ya jengo atahakikisha-

(a) anazuia uchafuzi wa hali ya hewa; na

(b) anaondoa na kutupa mabaki ya jengo alilobomoa, mahali alipoelekezwa kwa mujibu wa kibali.

Ada ya uzoaji taka

13. Halmashauri itawajibika kukusanya taka ngumu kutoka katika vizimba vya takataka vilivyoainishwa katika kila kata, na wazalishaji takataka watalipia ada au ushuru wa ukusanyaji wa takataka

kama ilivyooneshwa katika Jedwali la Tatu.

Ukusanyaji taka ngumu

14.-(1) Hairuhusiwi kuweka uchafu wenye asili ya maji maji kwenye pipa au chombo chochote cha taka ngumu au kitu chochote kinachoweza kulipuka na kusababisha madhara.

(2) Taka ngumu zote zitakazokusanywa kwenye pipa au chombo cha taka zitabaki kuwa mali ya mkazi au mmliki wa eneo lile mpaka zitakapokuwa zimefikishwa kwenye kizimba cha taka au zitakapokuwa zimetolewa na wakala kutoka katika eneo lake.

(3) Mtu atatakiwa kuwa na kibali cha Halmashauri ili kuchoma au kufukia taka ngumu.

Eneo la kutupa taka

15.-(1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa-

(a) kutenga eneo maalum kwa ajili ya kutupia taka;
(b) kuweka vyombo maalum vya kutunzia taka katika maeneo ya Halmashauri; na
(c) kutoa huduma ya uzoaji taka kwa malipo kutoka kwa wazalishaji wa taka hadi kwenye dampo.

(2) Serikali ya Kijiji itawajibika kutenga eneo la dampo kwa ajili ya utupaji wa taka ngumu.

Usafi katika kaya

16.-(1) kila mkazi, mwenye nyumba, mpangaji, au mmiliki atalazimika kuwa na choo na kupalilia majani na kufagia kila mara na kutunza mazingira safi kwa umbali wa futi kumi kutoka ukuta wa jengo kama ilivyo katika vipimo vilivyowekwa na kukubalika na Halmashauri.

(2) kila mkazi mwenye nyumba au mmiliki atapaswa kuweka jengo lake madirisha makubwa yasiyopungua 1/8 ya eneo la sakafu ya chumba au vipimo vilivyowekwa na kukubaliwa na Halmashauri

(3) Kila mkazi mwenye nyumba au mmiliki atalazimika kuwa na shimo la taka au pipa la taka

pembeni mwa nyumba yake na kuhakikisha taka hizo zinaondolewa au kuteketezwa mara pipa linapojaa.

(4) kila mmiliki wa biashara ni lazima kuwa na ndoo ya kunawia maji tiririka ikiwa pamoja na sabuni au kuwa na kitakasa mikono kwa ajili ya wateja wake.

Udhibiti wa taka maji

17. Mtu yeyote, kaya, taasisi, kampuni, kiwanda, ofisi, hoteli mgahawa na majengo yoyote wanapokusanyika watu, kama vile soko, minada, magulio, makanisa, misikiti, itatunza maeneo yake ikiwa ni pamoja na kufanya yafuatayo:

(a) kuwa na choo chenye hadhi inayokubalika kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii na kitahesabika kujaa kukisalia futi tatu kufikia usawa wa sakafu ya karo;
(b) choo kinatakiwa kujengwa umbali wa mita sitini kutoka katika kisima au chanzo chochote cha maji kinachotumika kwa matumizi ya nyumbani;
(c) kunyonya choo kikijaa kwa gharama zake mwenyewe;
(d) kuwa na kichanja kwa ajili ya kuanika vyombo baada ya kuoshwa.

Machinjio

18. Kila mtu atatakiwa kupeleka mfugo au mifugo yake machinjioni au mahali huduma hiyo inapopatikana na itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinja mfugo au mifugo mahali pengine popote ambapo sio machinjio, isipokuwa kwa kutoa taarifa kwa Afisa Mwidhiniwa na atalazimika kulipia gharama za machinjio.

Wajibu wa mmiliki wa duka la kuuza nyama

19. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa duka la kuuzia nyama kuhakikisha kwamba-

(a) ana jengo la kudumu lililosakafiwa na kuwekwa marumaru nyeupe kwenye sakafu na kuta kwa urefu wa futi sita kutoka usawa

wa sakafu;
- (b) jengo lina maji safi, gogo na misumeno ya kukatia nyama;
- (c) kuna pipa la kuhifadhia taka;
- (d) muhudumu ana koti jeupe pamoja na viatu vyeupe aina ya buti;
- (e) muhudumu anapima afya kila baada ya miezi sita.

Wajibu wa kushiriki shughuli za usafi wa mazingira

20.-(1) Kila jumamosi ya kila mwisho wa mwezi itakuwa ni siku maalamu ya kufanya usafi wa mazingira katika maeneo yote ya Halmashauri.

(2) Itakuwa ni wajibu na lazima kwa kila mwananchi kushiriki usafi wa mazingira kwa siku iliyopangwa na Halmashauri katika maeneo yao na maeneo ya umma.

(3) Kila mtu atahakikisha-
- (a) eneo lake la makazi na linalomzunguka;
- (b) eneo analofanyia biashara;
- (c) eneo la wazi lililokaribu naye kwa umbali wa mita kumi; na
- (d) eneo la mazingira ya ofisi,

ni safi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(4) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa jengo au kiwanja au eneo lolote ambalo halijaendelezwa kufanya usafi katika eneo hilo mara kwa mara.

Vikundi vya usafi

21. Halmashauri itahamasisha uundaji wa vikundi jamii na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira katika vijiji na vitongoji baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

Marufuku

22. Ni marufuku-
- (a) mtu yeyote kuendesha biashara ya upulizaji

dawa au biashara ya kuua wadudu au wanyama waharibifu katika nyumba yoyote au mahali popote bila cheti cha taaluma kinachotambuliwa na Serikali na leseni kutoka Halmashauri;

(b) mfanyabiashara yeyote kupanga bidhaa nje ya jengo lake la biashara, barabarani, vichochoroni au katika eneo lolote ambalo halikuidhinishwa kwa ajili ya shughuli hiyo;

(c) mfugaji kuruhusu mfugo au mifugo kuzurura ovyo mitaani au barabarani;

(d) mtu yeyote kutupa taka za aina yoyote barabarani au eneo lolote la wazi, kwenye vichochoro au kwenye chanzo chochote cha maji au katika eneo lolote ambalo halijatengwa kwa ajili ya shughuli hiyo;

(e) mtu yeyote aliye ndani ya gari kudondosha taka ngumu nje ya gari likiwa ndani au nje ya kituo cha magari na sehemu yoyote ile ambapo gari hilo linapita;

Sura ya 191

(f) mtu yeyote kuanzisha shughuli za kiwanda au mradi wowote unaoweza kuathiri mazingira bila kufanya utafiti wa mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

(g) mtu yeyote kuzuia maji kupitia njia yake ya asili kwa kujenga au kulima au kuweka kitu chochote kwenye njia ya maji kitakachoingilia mtiririko wa asili wa maji katika chanzo cha maji;

(h) mtu yeyote kuweka kitu chochote kwenye maji taka ambacho kinaweza kuathiri mtu yeyote au kuharibu mfumo wa tiba ya maji taka au kusababisha kuzuia mtiririko wa maji taka;

(i) mtu yeyote kulima kilimo cha matuta yanayosababisha maji kutuama ndani ya eneo la katikati ya mji;

(j) mtu yeyote kufanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo kwenye maeneo ya Halmashauri bila kibali;

(k) mtu yeyote kuegesha gari bovu kwenye njia ya miguu, mtaa, uchochoro, mtaro, maeneo ya wazi, barabarani na kusababisha adha kwa wakazi au watumiaji wa njia hiyo;

(l) mtu yeyote kuchinja au kuuza nyama ya aina yoyote katika maeneo yasiyokuwa machinjio au maduka ya kuuza nyama au katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri.

Makosa

23. Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hii kwa mtu yeyote-

(a) kujenga choo umbali usiozidi mita sitini kutoka kisimani, bwawani, mtoni, au chanzo cha maji yanayotumika, kwa matumizi ya binadamu;

(b) kutoa kinyesi au kusababisha kinyesi, mkojo, au taka maji yenye kinyesi kutoka kwenye choo chake au bafu lake au karo la kuoshea vyombo au nguo au kutoka kwenye bomba lolote linalochukua taka maji na kuyatitirisha kwenye barabara, mitaa, au kwenye mifereji ya maji ya mvua, au mfereji wowote ulio wazi;

(c) kutupa taka au kusababisha mtu mwingine atupe taka mahali popote pasiporuhusiwa na Halmashauri;

(d) kutiririsha maji taka barabarani, ziwani, mashambani, mitaani au katika eneo la nyumba ya jirani, mitaro ya barabara au eneo la wazi;

(e) kuendesha mashine ya kusaga na kukoboa katika jengo ambalo halijatekeleza masharti ya afya;

(f) kuuza nyama iliyotundikwa chini ya mti,

kuuza nyama ya mnyama aliyechinjwa bila kibali cha Afisa Mwidhiniwa au kwenye bucha ambalo sio safi na halijatekeleza masharti kama yalivyo katika Sheria Ndogo hii;

(g) kuuza chakula katika eneo ambalo halijatengwa au kusajiliwa kwa ajili ya shughuli hiyo;

(h) kuzika maiti katika eneo ambalo halikuainishwa kwa shughuli hiyo bila taarifa maalum kwa Afisa Mwidhiniwa;

(i) kutolipa ushuru wa kuzoa taka;

(j) kufanya biashara ya kuuza vyakula vya aina yoyote barabarani, mitaani na nje ya majengo bila kuweka ndani ya chombo safi chenye mfuniko;

(k) kuchezesha michezo au kuonesha michezo au burudani katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri;

(l) kuegesha gari bovu na kuliacha kando ya barabara au kichochoroni au eneo la wazi ambalo halijaidhinishwa kwa shughuli za gereji na kuliacha zaidi ya siku moja;

(m) kulima kandokando au ndani ya mita sitini kutoka kwenye chanzo cha maji;

(n) kutokuwa na pipa au chombo cha taka chenye mfuniko katika eneo la biashara;

(o) kutokuwa na choo au kukutwa na choo kibovu au kilichojaa;

(p) kukutwa na shimo la taka maji lililojaa au ambalo halina mfuniko;

(q) kusafirisha nyama bila kutumia gari ya kusafirishia nyama ambayo imekaguliwa na kupewa kibali cha kusafirisha nyama kwa ajili ya matumizi ya binadamu;

(r) kutoshiriki katika zoezi la usafi kiwilaya kila siku ya alhamisi ya kila mwisho wa mwezi

kulingana na mwongozo wa kitaifa wa zoezi hilo;

(s) kuziba kichochoro; na

(t) kutokuwa na chombo maalum cha kukusanyia takataka ndani ya gari la abiria.

Adhabu

24. Mtu yeyote atakayetenda kosa katika Sheria Ndogo hii, akitiwa hatiani, atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au vyote kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

25. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kwa mujibu wa Sheria, iwapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Nne.

## JEDWALI LA KWANZA

(*Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(1))*

ILANI YA KUZUIA AU KUKATAZA AU KUFANYA MAREKEBISHO

SEHEMU YA KWANZA

Ndugu…………wa Mtaa/Kijiji..…….Kaya ya…………Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika Tarehe………Mwezi………………Mwaka……………katika jengo au eneo lako la biashara/makazi/kutolea huduma/taasisi Namba … . iliyopo eneo la ……………...………………..katika kitongoji/Mtaa………………Kijiji cha…………. Kata ya……………

Imekuwa haina choo/choo kimejaa/kimeharibiwa hivyo unaamriwa kutekeleza mambo yafuatayo:

1. ……………………………………………………………………
2. ……………………………………………………………………
3. ……………………………………………………………………
4. …………………………………………………………………...

SEHEMU YA PILI

Unapewa muda wa siku ……………….. kuanzia tarehe ya kupokea ilani hii ili kutekeleza maelekezo yote yaliyoelezwa katika sehemu ya I ya ilani hii.

SEHEMU YA TATU

Ukaguzi wa kuthibitisha utekelezaji wa maelekezo uliyopewa utafanyika tarehe…………………… endapo utashindwa kutekeleza maelekezo ndani ya muda uliopewa Halmashauri itachukua hatua za kisheria bila kukupa taarifa nyingine.

| IMETOLEWA NA | IMEPOKELEWA NA: |
|---|---|
| Jina…………………………… | Jina………………..… |
| Saini…………………….. | Saini………………………… |
| Wadhifa…………………………… | Wadhifa……………………….. |
| Tarehe…………………………... | Tarehe………………………… |

*Futa lisilohusika

ILANI YA KUONDOA KERO

SEHEMU YA KWANZA

Ndugu……………………………………..wa Mtaa/Kijiji………………………….Kata ya…………………………Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika tarehe………mwezi…………mwaka…………katika jengo lako la biashara/makazi/kutolea Huduma/taasisi/kiwanja iliyopo eneo la …………………...

Pamekutwa na machukizo/kero/uchafu kama ifuatavyo:

1. ..……………………………………………………………………
2. ..……………………………………………………………………

3. ..………………………………………………………………………

SEHEMU YA PILI

Kwa ilani hii unaamriwa kurekebisha/kuondoa/kusafisha kwa:

1. ..………………………………………………………………………
2. ..………………………………………………………………………
3. ...…………………………………………………………………...

SEHEMU YA TATU

Unapewa muda wa siku ……………. tangu siku ya kupokea ilani hii, unatakiwa kutekeleza yote yaliyoelezwa katika sehemu ya II ya Ilani hii, kushindwa kwako kutekeleza ndani ya muda uliopewa Halmashauri italazimika kukuchukulia hatua kali za kisheria bila kukupa taarifa nyingine.

IMETOLEWA NA : IMEPOKELEWA NA :

Jina…………………………………Jina……………………

Saini………………………………..Saini……………………

Wadhifa……………………………Wadhifa…………………

Tarehe……………………………....Tarehe……………….....

JEDWALI LA PILI

ADA YA UPIMAJI WA AFYA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 8(1))*

| Namba | Aina ya Biashara | Kiwango cha Ada kwa Shilingi |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba ya starehe (baa, vilabu vya pombe za kienyeji na nyumba ya kulala wageni | 5,000/= kwa kila mfanyakazi/Mhudumu |
| 2. | Duka la bidhaa | 3,000/= kwa kila mfanyakazi/Mhudumu |
| 3. | Nyumba ya kutengeneza na kuuzia vyakula na au nyama choma. | 5,000/= kila mfanyakazi/Mhudumu |
| 6. | Duka la nyama | 5,000/= kwa kila mfanyakazi/Mhudumu |
| 7. | Viwanda vya kati | 3,000/=Kwa kila mfanyakazi/Mhudumu |
| 8. | Viwanda vidogo vya vyakula | 5,000/= kwa kila mfanyakazi/Mhudumu |
| 9. | Mhudumu wa chakula | 5,000/= kila mfanyakazi/Mhudumu |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 13)*

Ushuru wa Uzoaji Taka ngumu

SEHEMU A

| Namba. | Eneo | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) kwa mwezi |
|---|---|---|
| 1 | Kaya moja | 2,000/= |
| 2 | Maduka la rejareja | 5,000/= |
| 3 | Mashine ya kukamua mafuta ya alizeti | 5,000/= |
| 4 | Maduka la jumla | 10,000/= |
| 5 | Migahawa(Restaurant) | 5,000/= |
| 6 | Mashine za kukoboa au kusaga | 5,000/= |
| 7 | Vilabu vya pombe za kienyeji, baa, grocery, | 5,000/= |
| 8 | Mama lishe au Baba lishe, Nyama choma au chipsi | 2,000/= |
| 9 | Viwanda vya uselemala na mashine za mbao | 5,000/= |
| 10 | Bucha(Maduka ya Nyama, samaki) | 5,000/= |
| 11 | Nyumba za kulala wageni | 10,000/= |
| 12 | Saluni (Ususi/Vinyozi) | 5,000/= |
| 13 | Gereji ndogo | 5,000/= |
| 14 | Gereji kubwa | 10,000/= |
| 15 | Godown (Ghala) | 10,000/= |
| 16 | Kituo cha kuuza mafuta (Filling station) | 10,000/= |
| 17 | Ofisi za Taasisi mbalimbali | 5,000/= |

*Tangazo La Serikali Na. 466(Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 18 | Hospitali | 15,000/= |
| 19 | Vituo vya Afya | 10,000/= |
| 20 | Zahanati | 5,000/= |
| 21 | Shughuli za ushonaji | 2,000/= |
| 22 | Vioski au ibanda vya biashara | 2,000/= |
| 21 | Viwanda vikubwa | 10,000/= |
| 22 | Viwanda vidogo | 5,000/= |
| 23 | Wauzji wa mbao | 10,000/= |
| 24 | Kumbi za starehe | 10,000/= |
| 25 | Mafundi Vyuma | 5,000/= |
| 26 | Stoo za Mkaa | 5,000/= |

*Tangazo La Serikali Na. 466(Linaendelea)*

SEHEMU B

| Namba | Maeneo ya Uzalishaji Taka<br><br>Senta za Vijiji vya Busekela, Bukima, Kome, Rusoli, Murangi, Masinono, Saragana, Suguti, Kusenyi, Kwikuba, Mugango, Bwai KuUvinza, Busekela, Rukuba na Etaro | Kiwango cha Ushuru kwa Shilingi |
|---|---|---|
| 1. | Duka la rejareja | 500/= |
| 2. | Duka la jumla | 1,000/= |
| 3. | Biashara ya huduma | 2,000/= |

JEDWALI LA TATU

_____________

*(Limetengenezwa Chini ya kanuni ya 25)*

_____________

KUFIFILISHA KOSA

Mimi;……………………………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya;……………………………………..…….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Uvinza, kwamba mnamo tarehe;…… ya Mwezi;….…. Mwaka;……..… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kanuni ya;….….. ya Sheria Ndogo ya (Afya na Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza, niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU:

Leo tarehe;…....... ya mwezi;………… mwaka;…………..

Jina:………………………………...…………………….

Saini:………………………...……………………………

MBELE YANGU :

Jin:………………………….………..……………………

Wadhifa:……………………………………………...…

Saini:…………………………………………………………

Tarehe:……………………………………………………….

*Tangazo La Serikali Na. 466(Linaendelea)*

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza imegongwa kwenye Sheria Ndogo hii kufuatia azimio lililopitishwa katika mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya Uvinza uliofanyika tarehe 18 mwezi Disemba Mwaka 2023 na kushuhudiwa Lakari hiyo ikigongwa mbele ya:-

ACLAND DOMINIC KAMBILI
*Mkugenzi Mtendaji /Mkurugenzi wa Halmashauri*
*Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza*

JACKSON FREDRICK MATESO
*Meya/Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya Uvinza*

NAKUBALI,

/

**L.S**

Dodoma,
25 Machi, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*